

Wakati wa uchunguzi

# UPATIKANAJI WA HIFADHI

- Ikiwa huwezi kurudi katika nchi yako kwa sababu si salama kwako, **unaweza kuomba hifadhi hapa**.
- Ikiwa uliwasili bila pasipoti au visa, ni lazima upitie **kaguzi 4 za uchunguzi**.

**Ikiwa una umri chini ya miaka 18 na uko peke yako, wajulishe maafisa hao wa polisi mara moja.**

Watakupea mtu anayeitwa **mlezi** ili akusaidie.

## UKAGUZI WA UTAMBULISHO NA USALAMA

- Afisa wa polisi au mlinzi wa mpakani atauliza **jina** lako, umri, **asili na maelezo ya safari yako**.
- **Watapiga picha na kuchukua alama za vidole** vya kila mtu aliye na umri wa zaidi ya miaka 6.
- **Unaweza kupekuliwa** na mali zako zinaweza kuchukuliwa hifadhiwa hadi baada ya uchunguzi.
- **Waonyeshe maafisa hati zako zote**, kama vile kitambulisho au cheti cha kuzaliwa, hata kama ni picha kwenye simu yako.

## UKAGUZI WA AFYA NA UWEZEKANO WA KUATHIRIKA

- **Daktari au muuguzi atakuchunguza ili kuona** kama una magonjwa na matatizo mengine ya kiafya.
- **Shiriki ripoti zako za matibabu** au kadi ya chanjo ikiwa unazo.
- **Wafanyakazi waliopokea mafunzo watakusaidia.** Waambie ikiwa una wasiwasi, huzuni, unaogopa au unatafuta wanafamilia wako.
- **Unachoshiriki kinahifadhiwa kwa faragha** na hakitashirikiwa na mamlaka za nchi yako.

7

Ukaguzi huo unaweza kuchukua kipindi cha hadi siku 7.
Wakati huu, utabaki mahali ambapo uchunguzi huo unafanyika.

## KUMBUKA

- Ikiwa umeomba hifadhi, mamlaka husika lazima ikusajili haraka iwezekanavyo.
- Omba wakili ili kupata ushauri na mkalimani ikiwa huelewi lugha hiyo. Watakusaidia bila malipo.
- Kila mtu anayefanya kazi hapa lazima akuhudumie kwa heshima.
- Shirikiana na maafisa hao na uwaombe waeleze wanachomaanisha ikiwa jambo lolote wanalosema halieleweki.
- Ikiwa unataka kurejea nchi mwako, waombe maafisa msaada ili ujifunze kuhusu chaguo zako.



© Shirika la Umoja wa Ulaya wa Masuala ya Hifadhi, 2025

euaa
EUROPEAN UNION AGENCY FOR ASYLUM